## TERM 2 HOLIDAY WORK

**MAAGIZO, JIBU MASWALI YOTE.**

(1.) **UFAHAMU**

soma taarifa hii kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini.

Ankole ni mahali panapopatikana sehemu ya magharibi mwa Uganda.Watu wanaotoka sehemu hii wanaitwa wanyankole. Wanyankole hawa kutoka jadi wamekuwa na namna yao maalumu ya kufunga ndoa kulingana na utamaduni wa Ankole. Na kwa hivyo. Kufunga ndoa kulingana na utamaduni wa Ankole.na kwa hivyo kufunga ndoa kwa wanyankole ni mchakato ambao huchukua kipindi cha muda Fulani

Kwanza mwanamume anayetaka kuoa (bwana harusi) humpata mpatanishi wa kufanikisha mipango yake ya ndoa ambaye kulingana na utamaduni wa ankole anaitwa katerarume. Katerarume huenda moja kwa moja kwa familia ya msichana wa kuolewa (bibi harusi) na kuwaambia mawazo ya bwana harusi kuhusu kumuoa msichana wao. Kazi ya katerarume ni kuhakikisha kwamba amewashawishi wazazi wa msichana kukubali kumuoza msichana.

Baada ya makubaliano ya wazazi wa bibi harusi, sasa wazazi wa bibi harusi sasa wazazi na jamaa wa bwana harusi hukutana na wale wazazi wa bibi harusi ili wakubaliane kuhusu ndoa. Walakini bwana harusi haruhusiwi kusema chochote; bali katerarume ndiye anaarifu kuhusu kila kitu.baada ya makubalianokati ya pande mbili, katerarume hupewa nafasi ya kuhalalisha pendekezo la ndoa kufanyika

Mwishowe, kunatokea mjadala kuhusu mahari ambapo bwana harusi anafichwa kwenye sehemu Fulani huku mjadasla kuhusu mahari ya posa ukifanywa. Baadaye, kama hakikisho, bwana harusi anakubaliwa kumchukua bibi harusi na kumwangalia vizuri ambapo anaombwa kulipiga ngombe au kama ishara ya kuheshimu familia ya bibi harusi

Kinachofuata ni karamuya kumuoza msichana ambayo katika utamaduni wa ankole huitwa kuhingira. Watu wa familia wa pande zote mbili huhudhuria kama washahidi. Katika karamu hiyo, jamaa na bibi harusi humpatia zawadi kama ishara ya kumpenda na kumuaga aende afunge ndoa vizuri.

Kikundi cha wavulana na wasichana ambao huitwa enshagarizi humsindikiza bibi harusi mpaka kwa bwana harusi kwa ndoa halali, kwa kipindi cha muda mchache mwanzoni inakuwa ni kazi ya shangazi kumfunza bibi harusi kwenye ndoa vizuri ili isiharibike na kuvunjika

MASWALI

1.Ankole inapatikana wapi?
2. Watu wanaotoka eneo hilo wanaitwa aje?
3. Kufunga ndoa kwa wanyankole huchukua nini?
4. Eleza mchakato unaofuatwa ili bibi na bwana harusi waoane katika jamii ya Ankole
5 Kwa kutumia maneno machache, eleza jinsi ndoa ya harusi hufanyika katika kabila lako

( 2 ). SHAIRI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

HESABU

Kuhesabu ni muhimu
Bila hesabu kukwama, ni lazima maishani
Na jifunzeni mapema,ama si hivyo huzuni
Kuhesabu ni heshima, binadamu jifunzeni
Kuhesabu ni muhimu
Anaye pesa huduma, kubwa na tutazameni
Walimu fanyenimema, na tusiibwe dukani
Tujue kila alama, ya hesabu duniani
Kuhesabu ni muhimu
Tumuombe Allahuma, na macho yawe makini
Na atujaze rehema, tuhesabu mileleni
Kuhesabu si dhuluma, kamwe sote tujueni
Kuhesabu ni muhimu
Marafiki wako wema, pia wote hesabuni
Na yako mipango myema, isiwe kama ya dunu
Na ingawaje mapema, kuhesabu fikirini

1. Unafikiri ni aina gani ya uandishi huo wa juu?.............................................................
2. Shairi lina beti ngapi kwa jumla?.........................................................................
3. Shairi lina mishororo mingapi katika kila ubeti?...........................................................
4. Shairi lina mizani mingapi katika kila mshororo?.........................................................
5. Shairi hili lina pande ngapi?,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,
6. Toa angalau sababu tano ya kusoma hesabu,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,,

( 3 ) INSHA

Nyumbani kuna watu wengi na kazi zao tofauti. Andika dayalojia kati ya mama na mtoto nyumbani.

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

( 4 ) Likizo ya muhula wa pili imekwisha na unapanga kurudi shuleni. Mama yako amekuomba bajeti ya vitu ambavyo utaenda nazo shuleni ili kuzitumia, Andaa bajeti ya shilingi elfu mia mbili.

(200,000)……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

MWISHO

KILA LA HERI